Toleo 72- Jumad II 1444 H / Januari 2023 M

# Jarida la UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Hazina ya 'Hustler': Tungo Nyengine Mpya ya Mfumo wa Kibepari Ulioshindwa Kusimamia watu Kiuchumi

**HABARI NA MAONI**
Katika Ubepari Miradi Yote ni Maficho ya Rushwa na Unyonyaji kwa Watu wa Kawaida

**MATOLEO**
Serikali ya Mpito katika Toleo lake la Pili ni Serikali ya Utendaji

**JIBU LA SWALI**
Kuwapa Hongera Wakristo na Makafiri Kwenye Sikukuu Zao




uqab.or.ke | uqab_htk | UQABMagazine

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Hazina ya 'Hustler': Tungo Nyengine Mpya ya Mfumo wa Kibepari Ulioshindwa Kusimamia watu Kiuchumi

Katika hatua ya kuwapa mikopo wafanya biashara wadogo wadogo ambao wamekuwa wakitaabika kuchukua mikopo katika benki kubwa, serikali imezindua mfuko wa fedha unaojulikana maarufu Hustler Fund ambapo baada tu ya uzinduzi huo takriban Wakenya milioni 17 tayari wamechukua mkopo huo kwa muda tu wa saa moja kwenye siku ya kwanza ya uzinduzi huo. Kipindi cha uregeshaji wa mikopo kitapunguzwa hadi siku 14 katika mpango unaoonekana kufungua dirisha kwa wafanyi biashara wadogo kupata mkopo wa bei nafuu. Mfuko huo uliozinduliwa, utaona wakopaji wa kiwango cha chini wakipata Sh 500 huku kiasi kikubwa zaidi cha nyongeza kitakuwa Sh 50,000 kwa riba ya asilimia nane.

**Harakati ya Hizb ut Tahrir Kenya ingependa kubaini yafuatayo:-**

Ukweli kwamba kumekuwa na benki zinazotoa mikopo hiyo hiyo ya riba na ambayo imezidisha ugumu zaidi kwa raia wa kawaida na hatimaye kuwanufaisha wale wakopeshaji (wadai), inathibitisha kufilisika kisera kwa siasa na uchumi wa mfumo wa Kibepari. Kwa hivyo hazina hii ya mikopo inayotolewa na serikali ya sasa si lolote ila ubadilishwaji majina mapya ya mikakati ile ile ya zamani hivyo katu haitotatua kimsingi matatizo ya kiuchumi ambayo yamekita mizizi ndani ya taasisi za kifedha za kibepari.

Chini ya mfumo unaotegemea pesa za makaratasi (Fiat-Monetary), ambazo kiasili hazina thamani ya kidhati ila tu kupitia kanuni za kiserikali, pesa imefanywa ni bidhaa inayouzwa kwa bei ya riba ambayo inatumiwa na mabepari kunyonya na kuzuia raia wa kawaida kujikomboa kiuchumi. Mienendo ya mfumo wa kiuchumi wa kibepari, Riba hubadilisha sura yake mbaya mara kwa mara kwa kubadilisha kauli mbiu kama hii ya sasa 'Hustler Fund'.

Matatizo ya kiuchumi ya raia hayatatatuliwa kwa kutegemea mfumo wa mikopo ya Riba bali ni kwa kupita utekelezwaji wa mfumo wa kiuchumi wa Kiislamu na hapo ndio matatizo hayo yatatatuka kwani umeharamisha vikali riba kwenye miamala yote ya kifedha. Fauka ya haya, kwa kuwa Uislamu unaangalia tatizo la kiuchumi ambalo linapaswa kushughulikiwa ni ugawaji/usambazaji wa rasilimali. Kwa maana hii Khilafah kama serikali huwajibishwa kuchukua sera za kiuchumi zinazolenga kudhaminia kila raia waweze kukimu mahitaji yao msingi sambamba na kuwawezesha kufikia kukimu mahitaji ya ziada.

Tamati tungependa, kunasihi kwa dhati jamii yote kujiweka mbali na miamala yote ya kifedha ya riba kwani Mwenyezi Mungu (swt) ameukemea kwa ukali uovu huu pale aliposema:

الَّذِينَ يَأْكُلُونَ الرِّبَا لاَ يَقُومُونَ إِلاَّ كَمَا يَقُومُ الَّذِي يَتَخَبَّطُهُ الشَّيْطَانُ مِنَ الْمَسِّ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ قَالُواْ إِنَّمَا الْبَيْعُ مِثْلُ الرِّبَا وَأَحَلَّ اللّهُ الْبَيْعَ وَحَرَّمَ الرِّبَا فَمَن جَاءهُ مَوْعِظَةٌ مِّن رَّبِّهِ فَانتَهَىَ فَلَهُ مَا سَلَفَ وَأَمْرُهُ إِلَى اللّهِ وَمَنْ عَادَ فَأُوْلَـئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ

**"Wale walao riba hawasimami ila kama anavyo simama aliye zugwa na Shet'ani kwa kumgusa. Hayo ni kwa kuwa wamesema: Biashara ni kama riba. Lakini Mwenyezi Mungu ameihalalisha biashara na ameiharimisha riba. Basi aliye fikiwa na mawaidha kutoka kwa Mola wake Mlezi, kisha akajizuia, basi yake ni yaliyo kwisha pita, na mambo yake yako kwa Mwenyezi Mungu. Na wenye kurudia basi hao ndio watu wa Motoni, humo watadumu."** [Al-Baqara: 275]


**Shabani Mwalimu**

**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya**

# HABARI NA MAONI
# Katika Ubepari Miradi Yote ni Maficho ya Rushwa na Unyonyaji kwa Watu wa Kawaida




**Habari:**

Hivi karibuni Shirika la Reli Tanzania (TRC) lilipendekeza nauli kwa njia za treni ya reli ya kisasa (Standard Gauge Railway) kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro zinazotarajiwa kuanza Februari, 2023.

**Maoni:**

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu nchini Tanzania (LATRA), nauli iliyopendekezwa na TRC kwa daraja la tatu itakuwa Tsh 24,794 kwa mtu mzima na Tsh 12,397 kwa watoto wenye umri kati ya miaka 4 hadi 12, ilhali kwa daraja la chini ni Tsh 29,752 kwa mtu mzima na Tsh 14,876 kwa watoto.

Kwa uhalisia, nauli hizi zinazopendekezwa ni kubwa mno ikilinganishwa na uwezo wa kiuchumi wa walio wengi ambao wanaishi chini ya mstari wa umaskini. Lakini zaidi ya hayo, wengi waliamini kwamba kuanzishwa kwa safari za treni ya kisasa (SGR) kungefanya huduma ya usafiri wa treni kuwa haraka na nafuu.

Inafahamika wazi kuwa watu wengi hawana uwezo wa kumudu bei hizo za juu ndiyo maana mwezi Mei 2022, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA), ilitoa mwongozo mpya wa nauli za usafiri wa mabasi kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro, ambapo nauli yaTsh 8,000 ilikuwa kwa mabasi ya kawaida, huku Tsh 11,000 kwa mabasi ya kifahari. Kwa hakika, nauli za sasa za SGR hazikuzingatia mahitaji ya watu, hali halisi ya umaskini na kutoweza kwao kulipa bei za juu, wala hazikuonesha hali ya kujali masuala ya kuhudumia watu.

Kwa upande mwingine, inapaswa kuzingatiwa kuwa suala la ununuzi wa mabehewa hayo ya treni ya umeme kwa ajili ya SGR ambayo yaliwasili Dar es Salaam Novemba 2022 lilizua tuhuma za ufisadi na ubadhirifu wa fedha za Umma. Iliripotiwa kuwa kila behewa liligharimu takribani Tsh 2.2 bilioni, lakini inaaminika kuwa bei halisi kwa kila behewa kuwa karibu Tsh milioni 800-900. Kenya ililipa sawa na Tsh milioni 980 kwa behewa kama hilo la SGR. Kwa hivyo, suala la kuwaminya na kuwatia dhiki watu wa kawaida kwa nauli ya juu haliepukiki, ili kulipa gharama na kuzalisha faida kubwa.

Huu ndio uhalisia wa mfumo wa kibepari, watu waliokabidhiwa, kuaminiwa na wenye mamlaka hawajali watu, katika kila mradi ni lazima kuwepo na rushwa na ubadhirifu, na mwisho mzigo wa kurejesha gharama ni wa watu wa kawaida wasiojiweza.

Ubepari haujali hali ya umaskini na kutomudu gharama kwa watu hata katika huduma muhimu, kwa sababu kitu pekee kinachothaminiwa ni faida peke yake.

Katika Uislamu, kila aina ya miradi ya maendeleo na miundombinu ni kwa ajili ya kutengeneza ajira, kuchochea utoaji wa bure wa huduma muhimu kwa watu au angalau kwa gharama nafuu wanazoweza kuzimudu bila kuathirika.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Said Bitomwa**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Tanzania**

# Serikali ya Mpito katika Toleo lake la Pili ni Serikali ya Utendaji ya Kutekeleza Ajenda ya Magharibi Kafiri Mkoloni, Hakuna Kheri Yoyote Inayotarajiwa Kutoka Kwake



Leo, Jumatatu tarehe 5/12/2022, katika Ikulu ya Jamhuri jijini Khartoum, muafaka wa makubaliano ya kisiasa ulitiwa saini kati ya wanajeshi na Baraza Kuu la Vikosi vya Kutangaza Uhuru na Mabadiliko. Jenerali Al-Burhan, ambaye ana uhusiano na Amerika, alilazimisha vikosi vya kisiasa vinavyohusishwa na Uingereza kufanya makubaliano ya kudhalilisha ili kurejea kwa mara nyengine tena kwenye viti vya utawala, ambavyo ni tupu kabisa na mamlaka halisi.

Makubaliano haya yalijengwa juu ya katiba ambayo ilizalishwa kwa haraka na Kamati ya Uongozi ya Chama cha Wanasheria mnamo tarehe 30/8/2022, ambayo vikosi vya kimataifa vilimiminika, na kuisifu kuwa ni waraka unaofaa kwa kuleta pamoja vyama. Katika taarifa ya pamoja, balozi za nchi tisa za Magharibi ziliipongeza; ikiwemo Marekani na Uingereza zilizoidhinisha rasimu hiyo ya katiba, na kusema: "Kanuni msingi zilizomo katika waraka wa wanasheria zitakuwa muhimu katika kufikia mfumo wa kutegemewa na imara wa serikali ya mpito yenye uongozi wa kiraia" (Sudan Tribune, 11/9/2022)

Mchuzi wa sumu umeivishwa kwa mikono ya wenyeji, baada ya nguzo mbili za kikoloni (Marekani na Uingereza) kukubaliana kuunda serikali ya mpito kulingana na rasimu ya katiba ya Jumuiya ya Kisekula ya Mawakili, ambayo inaasisi maisha kwa msingi wa hadhara ya Magharibi Kafiri, kuangamiza umoja wa nchi, na kuifungua Sudan kwa upana ili utajiri wake ufujwe na makampuni ya kibepari katika mabara yote, baada ya mikono ya watu wa nchi hii kufungwa pingu na kuzuiwa kutokana na mali yao.

**Enyi Watu wetu wa Sudan:**

Serikali ya mpito itakayoundwa kwa mujibu wa makubaliano haya ya kisiasa na katiba ya Chama cha Wanasheria, watu wa Sudan hawatanufaika nayo, kwa sababu ni serikali inayofanya kazi sawa na mtangulizi wake, iliyokuja kutekeleza ajenda ya mkoloni iliyotungwa katika tamko la kisiasa na katiba, kama ifuatavyo:

**Kwanza:** Kujitolea maisha kwa ajili ya hadhara ya Magharibi kafiri kwa kuondoa sheria na mifumo ya maisha kutoka kwa utawala wowote wa Shariah. Kinyume na mfumo wa Uislamu (Khilafah), makubaliano haya ya kisiasa yanabainisha katika Ibara ya (3) kwamba: [Sudan ni serikali ya kiraia, ya kidemokrasia, ya kifederali, ya kibunge ambayo ubwana wake uko kwa watu...], na inaeleza katika Ibara ya (6) kwamba: [Kudhamini uhuru na kushikamana na mikataba ya haki za binadamu, hasa mikataba ya haki za wanawake]

*Endelea... UK 5*

Hizi ni maana zile zile zilizoainishwa ndani ya katiba, ambayo inautabanni mfumo wa kidemokrasia wa Kikafiri katika Ibara ya (1/3), na badala ya ubwana kuwa kwa Sharia ya haki, katiba inaeleza kwamba ubwana uko kwa watu (Ibara ya 5), na. badala ya kushikamana na hukmu za Shariah, makubaliano hayo yanatoa hati ya haki za kimsingi na uhuru, katika Sehemu ya II kwa ukamilifu wake kuanzia Kifungu cha 7 hadi Kifungu cha 33, haitegemewi kufutwa au kuathiri maandishi ya Ibara ya (77/2). . Hati hii imekusudiwa kufisidi yale ambayo hayakuathiriwa na ufisadi wa zamani kuhusu wanawake, watoto na wanaume, kwa maagano na makubaliano ya kimataifa ambayo yanagongana na itikadi tukufu ya Kiislamu, kama vile CEDAW, Mikataba ya Haki za Mtoto, na mengineyo.

**Pili:** Kuangamiza umoja wa dola, kwa kupitisha mfumo wa shirikisho katika makubaliano ya kisiasa na katika kifungu cha 35 cha katiba. Mfumo wa Shirikisho hugawanya mamlaka na kuanzisha vyombo (maeneo) ambayo yanafanana zaidi na majimbo. Katiba inakwenda mbali zaidi kwa kueleza kuwa kila kanda itakuwa na katiba yake (Ibara ya 36/1), ambayo inalisha maeneo na makabila katika kupigania madaraka katika kanda hizo. Kinacho angamiza umoja wa dola ni kuufanya Mkataba wa Juba kuwa sehemu ya katiba (Ibara ya 4/2), ambayo ni makubaliano ambayo yalijikita katika kugawanya nchi katika maeneo matano ya kikanda au kikabila, na kuvunja umoja wa dola kwa kuweka mfumo wa Hawakeer (Kifungu cha 38/8); sababu kuu ya migogoro na mizozo ya kikabila na kikanda katika maeneo mbalimbali ya Sudan!

**Tatu:** Kuondoka kwa dola kutoka kwa wajibu wake wa kimsingi, kwa mujibu wa Shariah. Ambayo ni kushughulikia mambo ya watu kwa kuhakikisha utoshelevu wa mahitaji yao yote ya msingi, kama vile chakula, mavazi, nyumba, kutoa usalama, elimu, na huduma ya Afya kwao.

Kwa hiyo, masuala haya hayajajadiliwa kwenye makubaliano ya kisiasa na rasimu ya katiba ya mpito, hivyo unakuta ibara moja tu ya uchumi, na ibara moja ya huduma ya Afya, na ibara moja ya elimu, na ibara hizo hizo hazilazimishi wajibu wowote kwenye shingo ya dola! Kwa sababu katiba inatunga sheria kwa ajili ya ukusanyaji ushuru wa dola, sio hali ya ustawi wa dola.

**Nne:** Kuhusu uchumi, baada ya bingwa wa Mfuko wa Fedha wa Kimataifa na Benki ya Dunia (Hamdok) kutekeleza maagizo mengi ya mfuko huo; kuanzia kwa kuondoa ruzuku kwa bidhaa na huduma zote, kupunguza matumizi ya huduma za afya na elimu, kuwafanya watu kurithi bei za juu, umaskini, na ugumu wa maisha, Serikali ya Mpito inakuja na kutishia watu kuongeza kodi, na kupanua mwavuli wa kodi kulingana na maagizo ya bajeti ya mwaka wa 2023, ili kuwatoa wananchi kutoka katika mzunguko wa uzalishaji, ili mikono yao izuiliwe kutokana na utajiri wa nchi yao, iwasilishwe na wakubwa wa ukoloni katika Serikali ya Mpito kwenye sahani ya dhahabu hadi kwa mabepari walafi. Shirika la Viwanda lilitangaza kufungwa viwanda 5940 kati ya jumla ya 7350 kutokana na gharama kubwa za uzalishaji, pamoja na ongezeko la ada na forodha, kwa mujibu wa taarifa ya Shirika hilo (AFP). Hivyo basi, serikali ya mpito itazidisha umaskini, bei za juu, na ugumu wa maisha.

**Kwa watu wetu wa Sudan:**

Sunnah ya Mwenyezi Mungu imetaka mabadiliko yasitokee yenyewe, bali lazima yatanguliwe na fikra kuhusu maumbile ya mfumo unaobadilisha maisha yetu na kuyageuza juu chini, ili tunaongozwe kwenye mfumo mtukufu wa Uislamu na Khilafah yake kwa njia ya Utume. Kisha tufuate fikra na vitendo, ili Uislamu ufikie katika mamlaka safi na takatifu mikononi mwa watu wanyoofu wenye madaraka na ulinzi, tukimtegemea Mwenyezi Mungu, na kutafuta msaada kutoka Kwake, na kukata kamba za makafiri wakoloni, kuunganisha ardhi na mbingu, ili ushindi wa Mwenyezi Mungu (swt) utushukie:

**(إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ آمَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ)**

**“Hakika bila ya shaka Sisi tunawanusuru Mitume wetu na walio amini katika uhai wa duniani na siku watapo simama Mashahidi”** [Ghafir: 51].

**H. 11 Jumada I 1444** **Hizb-ut-Tahrir**
**M. : Jumatatu, 05 Disemba 2022** **Wilayah Sudan**

**JIBU LA SWALI**

# Kuwapa Hongera Wakristo na Makafiri Kwenye Sikukuu Zao



**Swali:**

Assalam aleykum wa rahmatullah wa barakatuh, ndugu yenu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Bahaa kutoka Palestina. Twamuomba Mwenyezi Mungu muwe na afya njema na nguvu.

Swali langu ni kuhusu kuwapa hongera Wakristo kwa sherehe zao na kushiriki nao, na kilichonisukuma kuuliza swali hili ni jibu la swali la Sheikh Taqiuddin al-Nabhani, Mwenyezi Mungu amrehemu, kuliruhusu hilo, hivyo nataraji kutoka kwenu ufafanuzi wa jambo hili. Pamoja nalo ni jibu la swali la Sheikh Taqi.

**Jibu:**

Waaleykum salaam wa rahmatullah wa barakatuh

Tumeshatangulia kujibu swali hili, na hili hapa jibu kwako:

(Ndugu mtukufu)

Waaleykum salaam wa rahmatullah wa barakatuh

Kuhusu swali lako kuhusu kuwapongeza Watu wa Kitabu katika sikukuu zao, kabla sijakujibu, nitakutajia baadhi ya matoleo yaliyotangulia yanayohusiana nalo:

[1- Ilitolewa hapo awali mnamo tarehe 1/30/1970: (- Ni ipi hukmu ya kuwazuru Wakristo kwenye sherehe na sikukuu zao, kuwatembelea wagonjwa wao, na kwenda katika mazishi yao? Na je, Muislamu anafanya nini anapowatembelea? Na hii ina uhusiano gani na Hadith tukufu, "لا تبادئوا اليهود والنصارى السلام... الحديث"؟" “Musianzeni kuwatolea salamu Mayahudi na Wakristo...hadith”?

Jibu: Imethibiti kuwa Mtume (saw) alimtembelea Yahudi mmoja alipokuwa mgonjwa, na imethibiti kuwa alisimama kwa ajili ya jeneza la Yahudi mmoja, na imethibiti kuwa yeye, Rehema na amani zimshukie, aliusia kuhusu madhimmi (raia wa dola ya Kiislamu wasiokuwa Waislamu). Hivyo haya yote na mfano wake ni dalili ya kujuzu kuwatembelea Wakristo katika sherehe zao na sikukuu zao na kuwazuru wagonjwa wao na kwenda katika mazishi yao na kuwapa rambirambi na yanayofanana na hayo. Ama Hadith “Musianzeni kuwatolea salamu”, hii ni makhsusi kwa salamu pindi mkikutana nao njiani, na ni andiko (nasw) katika salamu hivyo haijumuishi kitu chengine chochote. 23 Dhul Qi’dah 1389 – 30/1/1970)

2- Kisha ikatolewa mnamo tarehe 7/17/1976: (- Je, yajuzu kuwatembelea Wakristo na Mayahudi katika sherehe zao?

Jibu: Inajuzu kuwatembelea Wakristo kwa sababu ni

*Endelea... UK 7*

katika wema, nalo ni jambo linalojuzu. 17/7/1976)

3- Pia ilitolewa mnamo tarehe 16/1/2010:

(Inajuzu kuwapongeza Ahlul-Kitaab katika sikukuu zao, ama kusema kwetu “na kwenu” ni kana kwamba umefanya qiyas kwa yale yaliyotajwa katika Hadith kwa kuwaambia “wa alaykum” pindi wanaposema “assalam aleykum” ...

Lakini si hivyo, kwani yale yaliyotajwa katika Hadith ni jibu la kusema kwao “as-saam aleykum” na neno ‘as-saam’ ni kifo, andiko la Hadith hiyo katika Bukhari na Muslim kupitia kwa mama wa waumini, Aisha (ra), ambaye alisema: Kundi la Mayahudi liliingia kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) wakasema: Assaam aleykum (kifo kiwe juu yenu). Aisha asema: nilifahamu basi nikasema wa alaykum as-saam wa al-la’natu (nanyi pia kifo na laana viwe juu yenu. Akasema: kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akasema: مَهْلاً يَا عَائِشَةُ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الرِّفْقَ فِي الْأَمْرِ كُلِّهِ “Taratibu ewe Aisha, hakika Mwenyezi Mungu anapenda upole katika mambo yote.” Nikasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, je hukusikia waliyoyasema? Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akasema: **قَدْ قُلْتُ وَعَلَيْكُمْ** “Nilisema na juu yenu.” Na katika riwaya nyengine ya Muslim kupitia kwa Ibn Omar (ra), amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw): **إِنَّ الْيَهُودَ إِذَا سَلَّمُوا عَلَيْكُمْ يَقُولُ أَحَدُهُمْ السَّامُ عَلَيْكُمْ فَقُلْ عَلَيْكَ** “Pindi Mayahudi wanapokusalimieni, mmoja wao akisema: assamu aleykum (kifo kiwe juu yenu), basi sema: iwe juu yako.” Na kwa hivyo umeona kuwa hii ni kwa sababu wanasema "assaam aleykum" (kifo kiwe juu yenu).

Lakini wakisema neno jema la kutupongeza, basi tunalikubali kutoka kwao, wakisema: Idd yenu iwe yenye baraka, tunawaambia jibu zuri na sahihi, kama vile kusema shukrani kwa kupongezi hizo, na ahlan wa sahlan au mfano wa hayo katika majibu yasiyopingana na Sharia. 16/1/2010) Mwisho

Kutoka na haya, yanabainika yafuatayo:

1- Inajuzu kuwapongeza ahlu dhimma kwa sikukuu yao kwa maneno mazuri yasiyopingana na Sharia, kwa hivyo hatuisifii sikukuu yao, yaani hatusemi “Idd Mubarak” au mfano wa hayo.

2- Lakini hii ni kwa wale wanaotimiza masharti yafuatayo:

A- Kwamba wawe miongoni mwa watu wa dhimma wanaoishi miongoni mwa Waislamu katika nchi za Kiislamu na mkataba wa dhimma unawahusu kwamba wasiwasaliti Waislamu...

B- Kwamba wasitupige vita kwa sababu ya dini au wasiunge mkono kufukuzwa kwetu... kama ilivyokuja katika Aya tukufu...

- Ama dalili kuwa wao wawe katika ahlu dhimma, jibu la kwanza la tarehe 30/1/1970 linaeleza juu ya hilo: (Ilithubutu kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alimtembelea Yahudi mmoja akiwa mgonjwa, na ikathubutu kuwa alisimama kwa ajili ya jeneza la Yahudi mmoja, na ikathubutu kuwa yeye (saw), aliusia kuhusu madhimmi, hivyo yote haya na mfano wake ni dalili ya kuruhusiwa kuwazuru Wakristo katika sherehe zao na sikukuu zao, na kuwatembelea wagonjwa wao, na kwenda katika mazishi yao, na kuwafariji, na mengineyo...) Hii inaashiria kwamba kinachokusudiwa hapo ni watu wa dhimma, kwani walikuwa wakiishi miongoni mwa Waislamu na walikuwa katika dhimma yao. Kisha Yahudi ambaye alitembelewa na Mtume (saw) katika maradhi yake alikuwa akimtumikia Mtume ﷺ kama ilivyoelezwa katika Hadith ya Al-Bukhari 1356 kutoka kwa Anas, (ra) **أَنَّ غُلَاماً مِنَ اليَهُودِ كَانَ يَخدُمُ النَّبِيَّ ﷺ فَمَرِضَ، فَأَتَاهُ النَّبِيُّ ﷺ يَعُودُهُ، فَقَعَدَ عِندَ رَأسِهِ، فَقَالَ: أَسلِم. فَنَظَرَ إِلَى أَبِيهِ وَهُوَ عِندَ رَأسِهِ، فَقَالَ لَه: أَطِع أَبَا القَاسِمِ ﷺ. فَأَسلَمَ، فَخَرَجَ النَّبِيُّ ﷺ وَهُوَ يَقُولُ: الحَمدُ لِلَّهِ الذِي أَنقَذَهُ مِنَ النَّارِ.** “Kwamba kijana mmoja miongoni mwa Mayahudi, aliyekuwa akimtumikia Mtume (saw) alikuwa mgonjwa, basi Mtume (saw) akamjia na kumtembelea, akaketi mbele ya kichwa chake, kisha akamwambia: Silimu. Akamtazama babake naye yuko mbele ya kichwa kichwa chake, basi akamwambia: Mtii Aba Al-Qasim (saw), basi akasilimu. Mtume (saw), akatoka huku akisema: Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu aliyemuepusha (kijana) na moto.” Yote haya yanaashiria kuwa yaliyotajwa katika jibu la kwanza ni makhsusi kwa madhimmi.

- Ama dalili ya kuwa wasiwe ni wenye kutupiga vita kwa sababu ya dini na wala wasiunge mkono kutolewa kwetu... nk. Ni Aya tukufu:

**لَا يَنْهَاكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ لَمْ يُقَاتِلُوكُمْ فِي الدِّينِ وَلَمْ يُخْرِجُوكُمْ مِنْ دِيَارِكُمْ أَنْ تَبَرُّوهُمْ وَتُقْسِطُوا إِلَيْهِمْ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ * إِنَّمَا يَنْهَاكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ قَاتَلُوكُمْ فِي الدِّينِ وَأَخْرَجُوكُمْ مِنْ دِيَارِكُمْ وَظَاهَرُوا عَلَى إِخْرَاجِكُمْ أَنْ تَوَلَّوْهُمْ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ.**

**“Mwenyezi Mungu hakukatazini kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita katika dini, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu. Hakika Mwenyezi Mungu anakukatazeni kufanya urafiki na wale walio kupigeni vita, na wakakutoeni makwenu, na wakasaidia katika kufukuzwa kwenu. Na wanao wafanya hao marafiki basi hao ndio madhaalimu.”** [Al-Mumtahina: 8-9]

Anasema Ibn Kathir katika sababu ya kuteremshwa aya hii tukufu: (Na neno lake Mwenyezi Mungu (swt) **لا يَنْهَاكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ لَمْ يُقَاتِلُوكُمْ فِي الدِّينِ وَلَمْ يُخْرِجُوكُمْ مِنْ دِيَارِكُمْ** **“Mwenyezi Mungu hakukatazini kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu.”** yaani hakukatazini kufanya wema kwa makafiri ambao hawawapigi vita katika Dini, kama wanawake na wanyonge wao, **أَنْ تَبَرُّوهُمْ** **“kuwafanyia wema”** yaani kuwafanyia ihsan **وَتُقْسِطُوا إِلَيْهِمْ** **“kuwafanyia uadilifu”** yaani kuwa waadilifu **إِنَّ اللَّهَ**

*Endelea... UK 8*



Pepe: info@uqab.or.ke

يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ **“Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu”**... Imam Ahmad amesema: Aarim alitwambia, Abdullah bin Al-Mubarak alitwambia, Musab bin Thabit alitwambia, Aamir bin Abdullah bin Al-Zubayr alitwambia, kutoka kwa babake alisema: Kutayla alimjia binti yake Asma binti Abi Bakr na zawadi: Sinab, Aqtu (maziwa mgando) na samli, na hali yeye ni mshirikina, lakini Asmaa alikataa kupokea zawadi yake na kumuingiza nyumbani kwake, basi Aisha akamuuliza Mtume (saw) Mwenyezi Mungu Mtukufu akateremsha: لا يَنْهَاكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ لَمْ يُقَاتِلُوكُمْ فِي الدِّينِ **“Mwenyezi Mungu hakukatazini wale ambao hawakukupigeni vita katika dini”** mpaka mwisho wa Aya. Basi akamwamuru apokee zawadi yake, na kumuingiza nyumbani kwake.

Na kauli yake (swt): إِنَّمَا يَنْهَاكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ قَاتَلُوكُمْ فِي الدِّينِ وَأَخْرَجُوكُمْ مِنْ دِيَارِكُمْ وَظَاهَرُوا عَلَى إِخْرَاجِكُمْ أَنْ تَوَلَّوْهُمْ **“Hakika Mwenyezi Mungu anakukatazeni kufanya urafiki na wale walio kupigeni vita, na wakakutoeni makwenu, na wakasaidia katika kufukuzwa kwenu.”** Yaani: hakika anakukatazeni kuwafanya ni vipenzi watu hawa ambao wamekuwekeni kuwa maadui, wakawapiga vita na wakakufukuzeni, na wakasaidia kukufukuzeni, Mwenyezi Mungu amekukatazeni kuwafanya vipenzi vyenu na anakuamrisheni kuwafanyia uadui. Kisha akathibitisha adhabu kali kwa kuwafanya vipenzi, basi akasema: وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ . **“Na wanao wafanya hao marafiki basi hao ndio madhaalimu.”** Kama kauli yake: يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَى أَوْلِيَاءَ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ مِنْكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ إِنَّ اللَّهَ لا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ **“Enyi mlio amini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa ni marafiki. Wao ni marafiki wao kwa wao. Na miongoni mwenu mwenye kufanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wenye kudhulumu.”** [Al-Maida: 51].

Kwa hivyo, inajuzu kuwapongeza watu wa dhimma katika sikukuu zao kwa maneno yasiyopingana na sheria, na pia inajuzu kuwapongeza wasiokuwa watu wa dhimma miongoni mwa makafiri kwa maneno yasiyopingana na sheria, pongezi ni katika wema, lakini hili ni kwa sharti kwamba Aya hii tukufu iwe inatekelezeka juu yao, wawe hawatupigi vita katika Dini na watutoi majumbani mwetu na wakaunga mkono kufukuzwa kwetu لَا يَنْهَاكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ لَمْ يُقَاتِلُوكُمْ فِي الدِّينِ وَلَمْ يُخْرِجُوكُمْ مِنْ دِيَارِكُمْ أَنْ تَبَرُّوهُمْ وَتُقْسِطُوا إِلَيْهِمْ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ **“Mwenyezi Mungu hakukatazini kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita katika dini, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu.”** Na hivi sasa hao ni wachache...

Nataraji hili linatosheleza, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Zaidi Mwingi wa Hekima.

Ndugu Yenu,

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**
**10 Jumada al-Akhir 1443 H**
**13/01/2022 M**


Pepe: info@uqab.or.ke